
# BIASHARA YA KABONI

Tanzania ina takribani hekta milioni 48 za misitu lakini kiwango cha upotevu wa misitu hii ni hekta 469,420 kwa mwaka. Biashara ya kaboni ya misitu ni biashara inayoibuka duniani ambayo ni moja ya utaratibu wa kupunguza mabadiliko ya tabia nchi kupitia kupunguza upotevu na uharibifu wa misitu au kupanda misitu mipya. Hata hivyo, kuna uelewa mdogo kuhusu Biashara ya Kaboni ya misitu kwa Watanzania wengi. Hali hii inasababisha kutopata fursa zinazoletwa na biashara hii. Kwa hiyo, andiko hili linajibu baadhi ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara kuhusu Biashara ya Kaboni ya misitu.




***Mradi wa Biashara ya Kaboni ni nini?***
Mradi wa Kaboni maana yake ni mradi wowote unaotekelezwa kwa ajili ya kuzalisha *Viwango vya Kaboni* (Carbon credits) vinavyotambulika kimataifa

***Viwango vya Kaboni ni nini?***
Viwango vya Kaboni (Carbon credits) maana yake ni kiasi cha tani moja ya hewa ya Kabonidayoksaidi au kiasi kinacholingana na hicho cha hewa nyingine ya gesijoto kinachopunguzwa kwa ajili ya kuuzwa kwenye Biashara ya Kaboni.

***Viwango vya Kaboni ya Misitu vinazalishwaje?***
Shughuli zinazoweza kufanyika na kuzalisha Viwango vya Kaboni ya Misitu ni kama vile:

- **Upandaji Miti** maana yake ni kupanda miti kwenye ardhi ambayo kihistoria haijawahi kuwa na misitu;
- **Upandaji Miti Upya** maana yake ni kupanda miti ili kurudisha msitu kwenye ardhi ambayo kihistoria kulikuwa na msitu;
- **Kutunza misitu** maana yake ni kupunguza utoaji wa gesijoto kutokana na upotevu na uharibifu wa misitu na kutekeleza jukumu la uhifadhi, usimamizi endelevu na kuongeza kiasi cha kaboni ya misitu katika nchi zinazoendelea



Viwango vya Kaboni hukokotolewa kwa kutumia taratibu za kawaida za hesabu za misitu.

***Ni misitu ipi inafaa kwenye Biashara ya Kaboni?***
Misitu inayomilikiwa na Serikali, Halmashauri za Wilaya, Serikali za Vijiji, Taasisi au watu binafsi inaweza kuingizwa kwenye biashara ya Kaboni. Misitu hiyo inaweza kuwa ya asili au ya kupandwa.



***Msitu ni nini?***
Msitu ni aneo la ardhi isiyopungua ekari moja yenye miti yenye urefu au inayoweza kufikia mita tatu na iliyofunga kwa asilimia walau 10.



***Nani wananunua Viwango vya Kaboni?***
Ni mashirika, watu binafsi au serikali wanaotaka waonekane kuwa viwango vyao vya uzalishaji wa gesijoto wanavifanyia kazi ili kupunguza athari za mabadiliko ya tabia nchi.

***Je bei ya Viwango vya Kaboni ikoje kwa sasa?***
Bei ya Viwango vya Kaboni hubadilika kutegemeana na nguvu ya Soko na aina ya mradi. Kwa miradi ya misitu kwa ujumla bei ya Viwango vya Kaboni huanzia dola za Kimarekani 2 hadi 20 kwa tani moja ya gesijoto.

***Nifanye nini ili nijiunge na Biashara ya Kaboni?***
Mchakato wa kuanzishwa kwa biashara ya Kaboni umeainishwa kwenye Kanuni na Mwongozo wa Biashara ya Kaboni uliotolewa na Ofisi ya Makamu wa Rais mwaka 2022 na marekebisho yake. Nyaraka hizi zinapatikana kwenye tovuti ya Ofisi ya Makamu wa Rais https://www.vpo.go.tz/ au tovuti ya Kituo cha Kitaifa cha Kuratibu Kaboni https://www.ncmc.sua.ac.tz/tanzania-carbon-trading-regulations.

***Nani wa kuwasiliana naye unapohitaji msaada?***
Katibu Mkuu,
Ofisi ya Makamu wa Rais,
Eneo la Mtumba,
S.L.P. 2502, Barua pepe: ps@vpo.go.tz, Simu: (255) (22) 2163400-19 au (255) (75) 6140140
**40406 DODOMA.**

Mkurugenzi,
Kituo cha Kitaifa cha Kuratibu Kaboni,
Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo,
S.L.P 3000, Barua pepe: ncmctanzania@sua.ac.tz, Phone 255 23 2603511-4.
**MOROGORO.**